


# KUZALIWA UPYA – (SEHEMU YA TATU)

Pokea salamu zangu asubuhi ya leo. Natumai umwema katika Kristo. Tunaendelea kufuatilia undani wa mada ya kuzaliwa upya.

Kuzaliwa upya ni siri na pia ni muujiza.

Dakika moja mtu amepotea katika dhambi zake, akitangatanga gizani. Anakosa tumaini la uzima huu au umilele ujao. Kisha muda mfupi tu baadaye, anaweza kubadilishwa na Mungu kuwa kiumbe kipya. Nguvu ya dhambi na Shetani imevunjwa. Anapata tumaini la maisha haya na maisha yajayo. Hili ni fumbo kweli!

Kuna watu 'wazuri' ambao hukaa chini ya mahubiri ya Injili kwa miaka mingi – watu ambao wanaonekana kuwa karibu na ufalme wa Mungu lakini hawaingii kamwe. Na kisha kuna watu ambao wako katika hali ya giza kuu - mbali sana na Mungu, kwamba huwezi kamwe kufikiria inawezekana kwao kuokolewa kutoka kwa dhambi na Mauti.

Lakini basi Mungu hupenya na kuwakumbatia. Wanazaliwa mara ya pili.

Hoja yangu ni kwamba hatuwezi kujua kwa hakika kwamba ni nani atakaa gizani na nani atachagua Nuru. (Soma **YOHANA 3:18-20**).

Kwa miaka mingi tumeshiriki katika huduma ya Yesu (soma **LUKA 4:18-19**). Tumemwona Mungu akifanya mambo ya ajabu! Tumemwona akiwapa macho vipofu. Tumemwona akiponya mioyo iliyovunjika. Tumemwona akitoa mamia ya mapepo.

Tumemwona Mungu wetu mtenda miujiza akitoa fedha zinazohitajika, kuzidisha chakula, kusababisha magari yaliyoharibika kukimbia, kuleta mvua kutoka anga kavu, kugeuza mkondo wa dhoruba kali, na kutuokoa kutokana na kifo.

Lakini jambo la kustaajabisha zaidi ambalo nimeona katika miongo saba ni mtu anayepitia hali ya Kuzaliwa Upya.

Maisha ya kimwili husababishwa na kujamiiana kwa binadamu pamoja na matendo ya kiungu (**ZABURI 139**). Tendo la kiungu pia huzaa kuzaliwa kiroho. Mungu huzalisha Kuzaliwa Upya ndani ya mtu anayemwalika kufanya hivyo.

Katika **YOHANA 3:5** Yesu alisema, ni lazima uzaliwe kwa maji (kuzaliwa kimwili) na kwa Roho (kuzaliwa upya kiroho).

Nimesikia aina mbalimbali za shuhuda kuhusu jinsi Mungu amewaokoa watu:
- Watu wengi huiskia Injili, Roho huwaita, wao huitikia kisha wanapata kuzaliwa mara ya pili.
- Wengine huhangaika na mawazo kuhusu Mungu kwa miaka mingi kabla ya wakati wa 'kujisalimisha' kwa wito wake.
- Wengine 'humtafuta Mungu' kwa muda mrefu kabla yake 'kuwapata'.
- Kwa wengine mabadiliko ni ya upole na amani. Kwa wengine ni makubwa na yenye nguvu.
- Wengine waliokoka wakiwa watoto (kama mimi nilikuwa na umri wa miaka saba) na wengine wanazaliwa mara ya pili kwenye vitanda vyao vya kufa.
- Wengine huzaliwa mara ya pili wakiwa wachanga na baadaye kubadilika kuwa na imani ya kiutu uzima.
- Baadhi ya matukio ya Kuzaliwa upya hayaeleweki. Wakati fulani mimi na mke wangu tuliomba kwa ajili ya msichana mdodgo mwenye hasira na asiyemcha Mungu ambaye alijaribu kujiua. Alilala kwenye kitanda cha hospitali akiwa katika kifo cha ubongo kwa siku tatu. Kisha akaamka akiwa mzima na kuzaliwa tena na akaokoka!

Lakini katika hali hizi zote, kuna mpito kutoka kwa maisha ya zamani na kuingia maisha mapya.

Mungu wetu ni Mungu wa ajabu, muumbaji ambaye humfuatilia kila mtu kwa matumaini kwamba atamgeukia, kuungama dhambi zake, kukiri unyonge wake, kumpa moyo na maisha yake, na kuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

Wakati wa Kuzaliwa Upya mambo kadhaa hufanyika;

- Watu hupita kutoka Kifo na kuingia Uzimani - **WARUMI 5:17; 6:4; 6:23.**
- Wanafanya Agano Jipya na Muumba wao - **LUKA 22:17-20; WAEBRANIA 4:16; 9:15; 12:24.**
- Roho Mtakatifu huwageuza kuwa viumbe vipya – Roho Mtakatifu huja kukaa ndani yao – Roho Mtakatifu huchanganywa na roho zao za kibinadamu – **TITO 3:5**.
- Roho Mtakatifu anawabatiza katika Yesu – sasa wako 'ndani ya Kristo' na 'Kristo yu ndani yao' – **WARUMI 6:3-4**;
- Roho Mtakatifu anawaunganisha na jumuiya ya Watu wa Mungu, ambapo kila mmoja anachukua kazi yake katika Mwili wa Kristo - **1 WAKORINTHO 12**
- Roho Mtakatifu huwapa moyo mpya - moyo wa Yesu - **EZEKIELI 36:26**.
- Roho Mtakatifu anaanza kubadilisha mawazo yao kuwa nia ya Kristo - **WARUMI 12:2**.
- Dhambi zao husamehewa na sio watumwa wa dhambi tena - hawako tena chini ya utawala wa Shetani – **WARUMI 6:6-22**.
- Roho Mtakatifu huwapa utakatifu wa Mungu - **WAEBRANIA 2:11; 1 PETRO 2:5.**
- Roho Mtakatifu huwapa haki ya Yesu - **2 WAKORINTHO 5:21.**
- Kusudi ambalo Mungu aliwaumba linaanza kuamilishwa na Roho Mtakatifu - **2 WAKORINTHO 5:18-20**.
- Roho Mtakatifu anawaagiza kushiriki katika huduma ya Yesu - **YOHANA 14:12a.**
- Roho Mtakatifu hutoa karama ya msingi ya kiroho (**WARUMI 12:6-8**) na Anazidisha kuwezesha 'karama za nguvu' za Roho (**1 WAKORINTHO 12:7-11**) ili kuwasadia kufanya huduma ya Yesu.

Nina hakika unaweza kuongeza mambo ambayo umepitia ama ambayo umeshuhudia Mungu akifanya wakati wa Kuzaliwa Upya kwa wengine. Pia utapata vifungu vingi vya Biblia vya ziada ambavyo vitasaidia kila moja.

Na huu ni mwanzo tu!

Huu ni mwanzo wa maisha mapya ndani ya Kristo Yesu ambamo tunabadilishwa hatua kwa hatua kuwa sura ya Yesu (**2 WAKORINTHO 3:18**).
Huu ni mwanzo wa uhusiano na Mungu ambao unaweza tu kukua na kuimarika na kukomaa - hadi tumwone uso kwa uso, na kubadilishwa kuwa kama yeye. (**1 WAKORINTHO 15**).

**WIKI IJAYO**: Tutajadili zaidi kuhusu kuishi maisha yaliyobadilishwa katika Kristo baada ya Kuzaliwa Upya.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.
Ni wako-




Douglas Van Devender.
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.